

Kumradhi SUMATRA

Katika gazeti hili toleo namba 617 la tarehe 9 hadi 15 mwezi Septemba mwaka jana, kulikuwa na habari iliyokuwa na kichwa kisemacho: Wenye mabasi, Sumatra ni rushwa juu ya rushwa.

Sumatra ni Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu.

Aidha katika habari hiyo iliyoongoza ukurasa wa mbele, kulikuwa na vichwa vidogo visemavyo: Madereva watoboa jinsi mgawo unavyotolewa.

Wasema maafisa Sumatra ni kama wana hisa. Wanapata mgawo kila ruti kama askari trafiki. Yabainika kuyafungia mabasi ni kiini macho, aibu. Wahoji kwanini wasubiri watu wafe ifungie mabasi!

Mara baada ya habari hiyo - kuteka - tulipokea



Omar Nundu

malalamiko kutoka Sumatra wakidhoji mambo kadhaa, ikiwemo uthibitisho wa madai hayo. Aidha wakati tunafanya uchunguzi wetu, Sumatra waliwasiliana nasi wakionyesha kuumizwa na habari hizo.

Inaendelea uk.3

Inatoka uk.1

Hivyo basi, na sisi kwa kuzingatia maadili ya uandishi wa habari na waledi, tulibaini kwamba habari hiyo ilijaa makosa na mapungufu mengi.

Hivyo kwa uungwana na unyenyekevu mkubwa, huku

Kumradhi SUMATRA

tukitambua kwamba Sumatra ni wadau wetu wa tasnia ya habari, tunachukua nafasi hii kuiomba radhi Menejimenti ya Sumatra, Wakarugenzi, wafanyakazi

na kila aliyeguswa na habari hiyo, akiwemo Waziri wa Uchukuzi Mhe. Omar Nundu.

Tunawahakikishia Sumatra na wasomaji wetu

kwamba makosa kama hay siku zijazo hayatajitokez tena. Hata hivyo tunapend kusisitiza kwamba lengo let halikuwa kuwaumiza Sumatra, na ndio maan tumeomba radhi.

-MHARIRI